TANGAZO LA SERIKALI NA. ……. la tarehe …….
SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

SHERIA NDOGO

(Zimetungwa chuni ya vifungu vya 6(1) na 16(1)

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI ZA MWAKA 2016

Jina na tarehe ya kuanza kuytumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi za mwaka 2016 na zitaaza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika katika eneo lote lililo chini ya Mamlaka ya Halmadhauri ya Manispaa ya Lindi.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakavyoelekezwa vinginevyo:-
"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolopwa kwa Halmashauri au wakala kwa niaba ya Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;
"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;
"Bidhaa" maana yake ni kitu chochote chenye thamani kitakacholetwa sokoni kwa lengo la kuuzwa;
"Ghala" maana yake ni sehemu yoyote iliyotegwa kwa ajili ya kazi ya kuhifadhi mazao ama bidhaa nyingine yoyote inayoweza kuuzwa au kununuliwa katika soko au gulio;
"Halmashuari" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotegwa na Halmshauri kwa ajili ya kuchinja wanyama na kuanika ngozi za wanyama waliochinjwa machinjioni hapo;
"Magogo" maana yake ni miti iliyokatwa yenye unene zaidi ya kipenyo cha sentimita ishirini na kuendelea na yenye mwelekeo wa kutoa mbao na bidhaa nyingine.
"Mkaa" ni pamoja na sehemu ya miti iliyochomwa na kukusanywa kwa pamoja kwa ajili ya matumizi ya kupika pamoja na shughuli nyingine;
"Mkataba " maana yake ni makubaliano ya ununuzi au uuzaji au utoji wa huduma yoyote kati ya Halmshauri na mdau husika;
"Mkurugenzi " maana yake ni Mkureugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa

yoyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;
"Mkulima" maana yake ni mtu yeyote, kampuni, taasisi au kikundi chochote kinachoshughulika na shughuli za kilimo cha mazoa ya chakula na biashara'
"Mnunuzi" maana yake ni mtu yeyote, taasisi yoyote inayoshughulika na ununuzi wa bidhaa ya aina yoyote;
"Muuzaji" maana yake ni mtu yeyote , kampuni, taasisi au kikundi chochote kinachoshughulika na uuzaji wa bidhaa ya aina yoyote; na
"Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa ajili ya vibali, leseni, na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halimshauri;

Ada na ushuru

4 –(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya huduma, vibali na leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri kama zilivyoainishwa kwenye sheria Ndogo hizi.
(2) Ada na Ushuru unaotozwa na Halmashauri utalipwa kabla ya huduma kutolewa.
(3) Endapo mtu yeyote atatakiwa kulipa ada au ushuru na atashidwa kulipa ndani ya muda uliopangwa, Halmashauri inaweza kukusanya ada au ushuru huo kwa njia ya mahakama.
(4) Pasipo kuathiri masharti yaliyowekwa katika kifungu kidogo cha 3 hapo juu, Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada au ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ada au ushuru pamoja na gharama za kukamata.
(5)Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada.

(6)Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka basi Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika isipokuwa uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa na kushikiliwa ambazo haziharibiki, itakuwa halali iwapo Mkurugenzi kwa maandishi atatoa taarifa ya kusudio la kuuza mali hizo iwapo mwenye mali atashindwa kulipa deni analodaiwa ndani ya kipindi cha siku kumi na nne (14).

(7) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.

Wajibu wa mfanyabiashara

5. –(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mfanyabiashara ;

(a) kuweka eneo analofanyia biashara katika hali ya usafi muda wote; na

(b) kulipa ushuru kama ilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(c) Kufanya biashara katika maeneo yaliyoruhusiwa na Halmashauri kwa

madhumuni hayo.

(2) Wafanyabiashara wote wa mazao ya misitu watauza mazao yao katika maeneo yaliyotengwa na Halmashauri kwa madhumuni hayo tu.

Uwezo wa Afisa muidhiniwa

6. Afisa Muidhiniwa atakuwa na uwezo wa :-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya ada na ushuru ;

(b) kumkamata bila hati ya kukamatia na kumshitaki mtu yeyote atakayeuza au kununua na kusafirisha bidhaa kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi ;

(c) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa bila kulipa ushuru.

Uteuzi wa Wakala

7. Halmashauri ina Mamlaka ya kumteua mtu binafsi, kampuni, asasi au taasisi kukusanya Ada na Ushuru kwa niaba yake.

Wajibu wa Wakala

8. Wakala aliyeteuliwa chini ya sheria ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:-

(a) kukusanya na kupokea Ada na Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa kiwango kilichoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote aliyokusanya kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala;

(c) Wakala aliyeteuliwa kukusanya mapato ya Halmashauri atatakiwa kweka dhamana sawa na marejesho ya mwezi mmoja au zaidi kabla ya kusaini Mkataba; na

(d) kumchukulia hatua za kisheria mtu yeyote ambaye atakiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa magari ya abiria kuingia kwenye kituo cha mabasi

9. Itakuwa ni wajibu wa kila basi la abiria kuingia katika kituo cha mabasi wakati wa safari zake lipitapo ndani ya mipaka ya Halmashauri.

Kukamata mali na kuuza

10. Mtu yeyote ambaye atakataa kulipa Ushuru au Ada ya mali yake kama ilivyo elekezwa na sheria hizi, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kukamata na kuuza mali hiyo kwa kibali cha mahakama.

Makosa

11. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote :-

(a) atakataa au atashindwa kutii agizo lolote atakalopewa na Afisa Muidhiniwa;

(b) atamzuia kwa namna yoyote ile Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi ;

(c) atakataa au atajaribu kukataa kulipa ada au ushuru anaopaswa kulipa ;

(d) atashawishi mtu au kundi la watu kukataa kulipa ada au ushuru ;

(e) atakwepa au atajaribu kukwepa kulipa ada au ushuru ;

(f) atauza au kununua mifugo nje ya eneo la mnada, soko au gulio ;

(g) atafanya biashara katika eneo lisiloruhusiwa ;

(h) atasababisha fujo kwenye mnada, gulio au soko; na

(k) atazuia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kumtoza faini mtu yeyote isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) iwapo mkosaji atakiri kwa maandishi kutenda kosa hilo kwa kujaza fomu maalum iliyopo kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi na kukubali kulipa faini anayodaiwa.

Adhabu

13. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili (12) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani kifungo na faini kwa kila kosa.

JEDWALI LA KWANZA

KODI ZA KUTUMIA MALI ZA HALMASHAURI

(Chini ya kifungu cha 4)

1. Wapangaji wa majengo ya Halmashauri

(a) Nyumba za Halmashauri.

Daraja la I	.....	Sh. 50,000/= kwa mwezi
Daraja la II	.....	Sh. 30,000/= kwa mwezi
Daraja la III	.....	Sh. 10,000/= kwa mwezi

(b) Ukumbi wa Halmashauri.

Shughuli za mikutano	Sh. 100,000/= kwa siku
Sherehe	Sh. 150,000/= kwa siku

(c) Vyumba vya biashara.

Soko kuu	Sh. 20,000/= kwa mwezi
Stendi Kuu	Sh. 70,000/= kwa mwezi
Uwanja wa Ilulu	Sh.20,000/= kwa mwezi
Bucha	Sh. 70,000/= kwa mwezi
Kujisaidia	Sh. 300/= kwa mtu
Kuoga	Sh. 500/= kwa mtu

(d) Vizimba/meza ..... Sh. 10,000/= kwa mwezi

(e) Biashara Ndogondogo ..... Sh. 200/= kwa siku

2. Kutumia Mitambo ya Halmashauri.

(a) Kijiko ..... Sh. 600,000/= kwa siku

(b) Lori ..... Sh. 400,000/= kwa siku

JEDWALI LA PILI

MAEGESHO YA MAGARI

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA GARI	KIWANGO CHA USHURU
1	Mabasi makubwa (abiria zaidi ya 30)	Sh. 500/= kwa saa
2	Mabasi madogo (abiria 20 hadi 30)	Sh. 300/= kwa saa
3	Mabasi madogo (abiria chini ya 20)	Sh. 200/= kwa saa
4	Malori (tani 7 na kuendelea)	Sh. 500/= kwa saa
5	Malori (chini ya tani 7)	Sh. 300/= kwa saa
6	Pickup	Sh. 200/= kwa saa
7	Magari madogo	Sh. 200/= kwa saa

JEDWALI LA TATU

ADA YA KITUO CHA MABASI

(Kwa magari ya biashara tu)

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA GARI	KIWANGO CHA USHURU
1	Mabasi makubwa (Zaidi ya abiria 30)	Sh. 4,000/= kwa safari
2	Mabasi madogo (Abiria 20 hadi 30)	Sh. 2,500/= kwa safari
3	Mabasi madogo (chini ya abiria 20)	Sh. 1,500/= kwa safari
4	Malori makubwa (tani 7 na kuendelea)	(Sh. 2,000/=) kwa safari
5	Malori makubwa (chini ya tani 7)	Sh. 1,000/= kwa safari
6	Pickup	Sh. 500/= kwa safari
7	Taxi	Sh. 1,000/= kwa siku
8	Pikipiki za magurudumu mawili	Sh. 1,000/= kwa siku
9	Pikipiki za magurudumu matatu	Sh. 1,000/= kwa siku
10	Magari madogo yasiyo ya abiria	Sh. 1,000/= kwa safari

JEDWALI LA NNE

HUDUMA ZA MAJI TAKA

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA HUDUMA	KIWANGO CHA USHURU
1	Kunyonya maji taka kwenye majengo ya biashara	Sh. 120,000/=
2	Kunyonya maji taka kwenye majengo ya makazi	Sh. 100,000/=
3	Kunyonya maji taka kwenye majengo ya taasisi	Sh. 80,000/=

JEDWALI LA TANO

ADA ZA HUDUMA YA MACHINJIO NA UKAGUZI

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA HUDUMA	KIWANGO CHA USHURU
1	Ng'ombe	Sh. 4,000/= kwa ng'ombe mmoja
2	Kondoo na mbuzi	Sh. 1,000/= kwa kondoo/= mbuzi mmoja
3	Nguruwe	Sh. 2,000/= kwa nguruwe mmoja
4	Kuku na jamii zote za ndege	Sh. 500/= kwa kila jamii ya ndege mmoja
5	Gari linalosafirisha nyama kutoka machinjioni	Sh. 500/= kwa ng'ombe
6	Cheti cha afya cha usafirishaji wa ngozi	Sh. 3,000/= kwa cheti kimoja
7	Ukaguzi wa mifugo	Sh. 10,000/= kila mkaguzi anapokwenda kukagua

		mifugo
8	Vibali vya kusafirisha mifugo:-	
	(a) Ng'ombe, mbuzi na nguruwe	Sh. 2,000/= kwa kila mmoja
	(b) Wanyama wengine	Sh. 250/= kwa kila mmoja
	(c) Leseni ya kusafirisha ngozi za wanyama zilizotengenezwa tayari kwa kuuzwa	Sh. 150,000/= kwa kila leseni

JEDWALI LA SITA

USHURU WA KUSAFIRISHA MAZAO MBALIMBALI

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA MAZAO	KIWANGO CHA USHURU
1	Korosho zinazosafirishwa nje ya Halmashauri pasipo kuongezwa thamani	5% ya bei ya kununulia
2	Mihogo	Sh. 500/= kwa kiroba
3	Nazi	Sh. 10/= kwa nazi moja
4	Ufuta, karanga na jamii ya kunde	5% ya bei ya kununulia
5	Mahindi, mtama na mazao mengine ya mafaka	5% ya bei ya kununulia
6	Chumvi	Sh. 10/= kwa kilo moja
7	Matunda	Sh. 500/= kwa kiroba
8	Mkaa	Sh. 500/= kwa kiroba
9	Mbao na magogo	Sh. 500/= kwa kiroba

JEDWALI LA SABA

ADA ZA UKAGUZI WA MICHORO YA RAMANI ZA MAJENGO

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	ENEO LA MSINGI LINALOZIDI MITA YA MRABA	ENEO LA MSINGI LISILOZIDI MITA YA MRABA	MAENEO YA KATI YA MJI NA VIWANDA (SH)	MAENEO YA MSONGAMANO WA CHINI (SH)	MAENEO YA MSONGAMANO WA KATI (SH)	MAENEO YA MSONGAMANO WA JUU (SH)
1		46.45		55,500/=	52,000/=	50,000/=
2	46.45	92.901	90,000/=	60,000/=	58,750/=	55,000/=
3	92.901	139.35	155,000/=	75,000/=	65,500/=	60,000/=
4	139.35	185.81	345,000/=	90,000/=	80,250/=	66,750/=
5	185.81	278.71	470,000/=	110,000/=	94,500/=	77,50/=
6	278.71	371.61	620,000/=	130,000/=	100,000/=	88,000/=
7	371.61	464.51	780,000/=	150,000/=	105,000/=	90,000/=
8	464.51	557.42	855,000/=	180,000/=	120,500/=	100,000/=
9	557.42	650.3	940,000/=	210,000/=	135,000/=	125,000/=
10	836.12	929.01	1,150,000/=	340,000/=	250,000/=	132,000/=
11	Malipo ya ziada kwa kila mita ya mraba inayozidi 92.901	92.901	22,500/=	18,500/=	15,000/=	10,000/=

JEDWALI LA NANE

ADA ZA VIBALI VYA UJENZI/UKARABATI WA MAJENGO

(Chini ya kifungu cha 4)

NA	AINA YA JENGO	KIWANGO CHA ADA (SH)
1	Jengo la makazi	15,000/= kwa kibali
2	Jengo la makazi ghorofa moja	50,000/= kwa kibali
3	Jengo la makazi zaidi ya ghorofa moja	100,000/= kwa kibali
4	Jengo la makazi na biashara	150,000/= kwa kibali
5	Jengo la biashara	200,000/= kwa kibali
6	Jengo la biashara zaidi ya ghorofa moja	250,000/= kwa kibali
7	Jengo la kiwanda	100,000/= kwa kibali
8	Jengo la taasisi	500,000/= kwa kibali
9	Vibanda vya biashara	50,000/= kwa kibali
10	Ujenzi wa uzio wa kudumu	1,000/= kwa mita
11	Ujenzi wa uzio wa muda	500/= kwa mita
12	Kukata barabara	25,000/= kwa mita
13	Maombi ya upimaji ardhi	20,000/= kwa kibali

Sheria ndogo hizi zilipigwa Muhuri wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kufuatia maamuzi yaliyopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 28 mwezi Aprili, 2016 mbele ya:-

J. M. Satura,
Mkurugenzi wa Manispaa.

Mohamed L. Lihumbo,
Mstahiki Meya wa Manispaa.

NAKUBALI

Dodoma

John Pombe Magufuli,
RAIS.

Tarehe:……..